voice of voiceless Msj72@ymail.com

# Msj weekly

Issue No.1 Morogoro school of journalism May 19 2017

**KEBWE:WAANDISHI TANGAZENI VIVUTIO VYA UTALII**

UK>>3



**SERENGETI BOYS KUIVAA ANGOLA**

UK>>14



# Salma :Wanachuo lipeni ada kwa wakati



Mratibu wa masomo chuo cha uandishi wa habari Morogoro Bi.Salma Zebedayo akiwa ofisini kwake

Wanafunzi wanaotarajia kufanya mitihani mwishoni mwa mwezi wa tano katika chuo cha Uandishi wa habari Morogoro (MSJ) wametakiwa kulipa ada mapema iwezekanavyo ili kuepukana na changamoti zinazoweza kuwapata ikiwemo kusimamishwa kufanya mitihani au kurudia kabisa masomo yao

***Inaendelea uk>>2***




MOROGORO SCHOOL OF JOURNALISM

MEDIA FOR DEMOCRACY

Published by Morogoro School of journalism (MSJ), under student organization (MOSJOSO)

# Salma :Wanachuo lipeni ada kwa wakati

Na:Linus Patrick

Hayo yamesemwa na mratibu wa masomo Bi.Salma Zebedayo alipokuwa akizungumza mapema na wanafunzi wa Astashahada mchepuo wa 52 na kuongeza kuwa kipindi hiki yeyote atakayekosa kuingia darasani kwa kipindi cha siku 21 kutoka sasa hatofanya mtihani badara yake atafanya mtihani maalumu(special).

Mratibu wa masomo ameendelea kwakusema kuwa wanafunzi inabidi watumie nafasi hii kuhakikisha wanakamilisha kila kitu ili muda wa kufanya mtihani kila mmoja aweze kuingia kweye chumba cha mtihani kwa kuwa ratiba ya mtihani imeshatolewa kwahiyo hawana budi kuifuata.

Mara baada ya mratibu kutoa maagizo hayo Gazeti la Msj weekly limeweza kuzungumza na wanafunzi wa Astashahada mchepuo wa 52,akizungumza kwa niaba ya wenzake Bw.Linus Patrick amesema kuwa"wao kama darasa wamejipanga na watahakikisha wanatimiza maagizo yote yaliotolewa ili kuepukana na



*Mratibu wa masomo chuo cha uandishi wa habari Morogoro Bi.Salma Zebedayo akiwa ofisini kwake*
*picha na Husna Rashid*

changamoto zinazoweza kujitokeza.

Aidha Bw.Linus ambaye pia ni kiongozi wa darasa(CR) aliongeza kuwa wanatoa shukurani zao za dhati kwa uongozi wachuo kwa ujumla na walimu wote waliowafundisha kwa kipindi chote na kufikia sasa ambapo wanajiandaa kwa ajili ya kufanya mitiani yao ya mwisho.

Pamoja na hayo wale waliokuwa hawajakamilisha michango yote wamesema hali hii inasababishwa na kutika katika familia zenye kipato cha chini huku na wengine wakiwa wanalipiwa na wahisani kwahiyo hali hii inasababisha kutolipa ada kwa wakati mwafaka.

Ikumbukwe kuwa wanaotarajia kufanya mitihani yao mwishoni mwa mwezi huu wakifahuru mitihani yao wanaweza kuendelea na masomo yao ya Stashahada(Diploma)chuoni hapo mwezi wa saba mwaka huu.

# Tatizo la maji lapata ufumbuzi

Na:Emilia Mandaki

Wanafunzi wa chuo cha uandishi wa habari Morogoro (MSJ) wanaoishi katika hosteli za chuo hicho wameondokana na shida ya maji ambayo imekuwa ikiwakabili kwa muda



*Wanabweni wakiwa katika hali ya furaa baada yakupata maji*

mrefu baada ya maji kuanza kutoka mfululizo bombani bila kukata.

Aidha wanafunzi hao wamekuwa wakikabiliana na shida ya maji takribani miezi nane mfululizo walidai kwamba bomba lao lilikata kutoa maji kwa kipindi kirefu huku wakishindwa kuelewa shida nini.

***Inaendelea uk>>4***





Published by Morogoro School of journalism (MSJ), under student organization (MOSJOSO)

Published by:
Morogoro school of Journalism
P.o.Box 1287,
Morogoro.

Website:www.msj.Ac.tz/www.mosjoso.com
Email:Msj72@ymail.com

Supervisors
Francis Mkude

Chief Editor
Meshack Rutta

Layout$ Design
Linus Patrick,
Anamalia $
Mathew Mtaba.

MEDIA FOR DEMOCRACY

# Fuatilia gari la shule la mtoto wako

Waswahili usema,"elimu ni ufunguo wa maisha" na "elimu haina mwisho". Hii inadhihirisha wazi kwamba bila elimu hujafanya chochote mahali ulipo.

Elimu kwa maana pana ni tendo au uzoefu wenye athari ya kujenga akili, tabia ama uwezo wa kimaumbile wa mtu binafsi. Katika dhana ya kiufundi, elimu ni njia ambayo hutumiwa makusudi na jamii kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine.

Walimu katika taasisi za elimu huratibisha elimu ya wanafunzi wao kupitia masomo kama vile ya kuandika, kusoma, kuhesabu (hisabati), sayansi na historia. Mbinu hii wakati mwingine huitwa masomo haswa tunaporejelea somo la aina fulani, kwa kawaida mbinu hii hutumiwa na maprofesa katika taasisi za masomo ya juu.

Kuna elimu maalumu kwa wale wanaohitaji ujuzi wa kitaaluma, kama vile wanaohitaji kuwa marubani. Juu ya hayo, kuna nafasi nyingi za elimu katika viwango vingine visivyo rasmi kama vile majumba ya ukumbusho, maktaba pamoja na mtandao na tajriba za maisha.

Hivi karibuni,kuna picha iliyoonesha watoto wa shule waliokuwa wamepakiwa kwenye gari moja ambalo lilikamatwa na askari wa usalama barabarani.

Gari hiyo ilikamatwa na askari wa kituo kikuu cha askari wa usalama barabarani kwa kuzidisha kiwango cha abiria; kitendo kinachohatarisha usalama wa watoto hao. Watoto hao walionekana wakishuka kwenye gari hilo aina ya Toyota Noah huku ikibainika, baadhi walikalishwa kwenye buti.

Gari hilo lenye uwezo wa kubeba abiria wanane, inasadikiwa lilikuwa na wanafunzi wapatao 30. Kweli haya siyo maajabu tu, bali ni hatari!. Tatizo la usafirishaji wa wanafunzi (watoto) katika hali isiyo salama, naamini ni kubwa kuliko inavyotegemewa.

Toyota hiyo ilioneshwa ikiwa imefunikwa turubai, ndani kukiwa na watoto ambao ilielezwa walikuwa wakitoka jasho kutokana na joto kubwa. Pamoja na hayo machache yaliyowahi kukamatwa na polisi, naamini wakiamua kufanya ufuatiliaji wa kina wa mfumo wa usafirishaji wanafunzi, wataini kasoro nyingi kwa shule nyingi; ikiwamo ubovu wa magari husika.

Hili ni kwa pande zote mbili; kwa maana ya magari ambayo wazazi wanaweza kuamua kuyatafuta wenyewe na kulipa mwenye gari, au magari yanayomilikiwa moja kwa moja na shule na wazazi hulazimika kuchangia gharama za usafiri.Wanachama wote wanashurutishwa kuhakikisha elimu kwa wote. Katika kiwango cha kimataifa, Mapatano ya Umoja wa Mataifa ya haki za kiuchumi, za kijamii na za kiutamaduni.

Si suala la kificho, baadhi ya magari hayo yenye nembo ya 'school bus', yamekuwa yakionekana barabarani yakiwa yamejaza watoto kupitia kiasi. Mengine mwonekano wake unadhihirisha wazi kuwa ni mabovu na hayana viwango vya kubeba watoto hao wa shule.

Kasoro nyingine ambayo baadhi ya shule zimekuwa zikifanni kuachia.

# KEBWE:WAANDISHI TANGAZENI VIVUTIO VYA UTALII

Aidha mkuu huyo aliendelea kuesma kuwa waandishi wa habari wote mkoani hapa wanafanya kazi zao wakiwa huru kwasababu hajawai kupokea kesi ya aina yoyote inayohusu kunyanyaswa kwa waandishi mkoani hapa,na kutaka waandishi wote kufanya kazi kulingana na maadili yanavyoelekeza kwasababu kuna baadhi yao wanatoa habari zisizo za muhimu wao wakidai heti wanatafuta engo ya kutokea .

Nakuongeza kuwa katika mkoa huu kuna zaidi ya viwanda 300 ila vilivyo vingi havijulikani kwasababu waandishi wa habari hawavitangazi nakuongeza kuwa katika nchi yetu hakuna mkoa wenye vivutio vya watarii kama mkoa huu,kwahiyo akawaomba wavitanagaze kwanguvu na kuachana na habari za kutafuta hengo.

Maazimisho hayo ambayo uazimishwa kila tarehe 3/5 kila mwaka yaliyoanza mnamo saa 10:15 kwa maandamano kutoka katika ofisi za chama cha waandishi wa habari mkoa cha MOROGORO PRESS CLUB(MPC) ambapo vituo vya redio vikiwemo vya Abood,TV Iman,Planet Fm,Sua Fm,Ukweli Fm na magazeti ya Mtanzania,Mwananchi,Majira pamoja na hayo vilikuwepo vyuo vinavyotoa taaluma ya Uandishi wa habari kama,chuo cha uandishi wa habari Morogoro(MSJ),Chuo cha St.joseph na Chuo kikuu cha kihislam.

Maandamano hayo yalichukua takribani masaa mawili mpaka kufika katika ukumbi wa New savoy uliokuwa u meandaliwa rasmi kwashughuli hiyo.

Mara baada ya ya utambulisho wakila aliyefika pale ilifuta hotuba na taarifa fupi kwa mgeni rasmi ambapo taarifa hiyo ilikuwa ikielezea kwa ufupi historia ya Club hiyo kuwa kutoka mwaka 2005 walikuwa wakikodisha ofisi hizo na kuongeza kuwa chama hicho kilianzishwa mwaka 1990 kikiwa na wanachama Tisa (9) kikiwa na lengo la kujenga mahusiano mema na waandishi wa habari na kuongeza wataaramu.

Pamoja na hayo waandishi wa habari waliweza kutoa kero zao kwa mgeni rasmi kuwa wamekuwa wakifanya kazi yao katika mazingira magumu kwakuwa wananchi hawawapi hushirikano wa kutosha na mara pengine kutishia maisha yao na kusababisha kufanya kazi kwa hofu kubwa na kumwomba mkuu huyo kuwapa ulinzi wakutosha.

Mkuu huyo ndipo alisimama na kuwashukuru kwa taarifa hiyo na kuwaptia kiasi cha shilingi laki tano (500000/=Tsh) na kuongeza kuwa kuhusu usalama wao atalishugulia.

Hatimaye mwenyekiti wa Club hiyo akwakumbusha kuwa maazimisho hayo kitaifa yamefanyika mkoani Mwanza na duniani ni katika mji wa Jakatta-Indonesia na bada yakusema hayo kuhairisha shuguli hizo na kuwatakia waandishi wa habari pamoja na wanafunzi kazi njema na kuongeza kuwa yote yaliojadiliwa wayawanyie kazi.



*Mkuu wa mkoa Mh.Kebwe S.Kebwe akiutubia siku ya uhuru wa vyombo vya habari picha na Yasinta Maarifa. Watu 2 wajeruiwa katika ajali picha na Yasinta Maarifa*

## JE ? WAJUA

Tanga ndio mkoa wenye matunda mengi kuliko mikoa yote Tanzania ,ikiwemo matunda yanayo patikana porini matunda hayo yamefanyiwa utafiti kwa miaka takribani 63 iliyo pita baada yakuona matunda yaporini kuwa chakula cha ndege .

Matunda hayo yamegawanyika katika makundi mawili,matunda yenye mbegu ndani na yasiyo na mbegu, yamegudulika kuwa nichanzo kikubwa cha kuongeza vitamin kama vile vitamin A,B,C,E ambazo kwa mwili wa bina damu ni muhimu kwajili ya kuupa mwili unzi dhidi ya magonjwa

# Watu 2 wajeruiwa katika ajali

Na,Laula Gasper

Watu wawili wajeruhika na kukimbizwa hospitarini akiwemo dereva wa gari moja katika ajari mbaya iliyotokea maeneo ya Nanenane kata ya Tungi manispaa ya Morogoro.

Ajari hiyo iliyotokea mnamo Tarehe 28/4/2017 majira ya saa 8:30 iliyohusiha Magari mawili aina ya ICE yaliyogongana uso kwa uso yenye Namba za usajiri T-220 ADF na T-572 AKY yanayofanya safari zake Morogoro-Tungi,Tungi-Morogoro .



*Mabasi madogo aina ya Hiace yaliyopata ajali eneo la Nanenane picha na Zaituni*

Wakiongea na Msj weeklly katika nyakati tofauti abilia waliokuwa wakisafiri wamesema chanzo cha ajari hiyo ni Mvua kubwa zinazoendelea kunyesha na kuongeza kuwa uchakavu wa barabara ndio hasa uliochanigia kwa kiasi kikubwa kutokea kwa ajari hiyo na barabara kuwa finyu hivyo kushindwa kupishana na kusababisha magari hayo kugongana uso kwa uso.

Akidhibitisha kutokea kwa ajari hiyo mkuu wa kituo kidogo cha polisi kilichopo maeneo ya Nane nane,kata ya tungi ,Manispaa ya Morogoro amesema kuwa ,katika ajari hiyo iliyotokea majira ya saa 08:30 za asubuhi imesababishwa na miundombinu mibaya ya Barabara na mvua zinazoendelea kunyesha. Akaongeza kuwa na uzembe wa madereva unachangia kwasababu walikuwa wakitumia barabara hiyo kwa kipindi kirefu na wanajua matatizo yake ila muda mingine wanaendesha magari hayo kwa kasi na kuweka hatarini maisha ya Abilia.

Pia akawataka kubadikika ili kuweza kuzuia ajari zisizo za lazima ikiwemo na kufanyia marekebisho magari yao yaani( service) kwasababu yanaonekana kuwa yanafanya kazi kwa muda mrefu pasipo kuyarekebisha .

Naye mganga mkuu wa hospitali ya mkoa amethibitisha kupokea majeruhi hao wawili na kusema kuwa hali zao siyo mbaya na wanaendelea vizuri na hali ikiendelea kuwa nzuri wataweza kuruhusiwa muda wowote na kurudi nyumbani.

# Tatizo la maji lapata ufumbuzi

Inatoka Uk..2

Akizungumza mmoja wa wanafunzi hao veronicaNade alisema kuwa kwa kipindi kirefu tumekuwa tukihangaikia kutafuta maji tena kwa gharama ambayo ilikuwa inafanya kuongeza bajeti ya matumizi chuoni hapo " Hapo awali tulikuwa na shida ya maji tulikuwa tunahangaika kutafuta maji tena kwa gharama dumu moja la maji shilingi mia tano jambo ambalo lilituongezea bajeti ya matumizi lakini kwa sasa tuna maji mengi mpaka tunafurahia chuo.



*Wanabweni wakiwa katika hali ya furaa baada yakupata maji*

Naye kiongozi wa hosteli Yasinta Maalifa alisema kuwa shida ya maji ilikuwa tatizo sugu kwa wanahosteli ambalo limetutesa kwa muda mrefu na limekuwa likitunyima raha kwa sababu karibia kila kazi inahitaji maji hay ohayo yalikuwa yanakosekana kwa lipindi cha muda mrefu" kwa kweli maji yalikuwa yakitunyima raha na wengi wetu kuichukia chuo kama unavyojua maji ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu.

Aliendelea kusema hakika sasa tunamshukuru mungu kwa kutuwezeshea upatikanaji wa maji kwani tunaisi furaha yetu imerudi kwa kasi tunaishi kwa raha , pasipo na ghasi yoyote na chuoni tunasoma bila mawazo ya maji.

Wanafunzi hao waliishukuru Msj weekly kwa kuwatembelea hosteli hapo , hivyo wanafuraha shida ya maji imekoma na hivyo watasoma kwa raha pasipo mawazo .

MOROGORO SCINATOKA UK..2

MEDIA FOR DEMOCRACY

Published by Morogoro School of journalism (MSJ), under student organization (MOSJOSO)

# Maandalizi Nanenane ya pambamoto

Na,Meshack Rutta

Wakulima na wafanya biashara wakubwa na wadogo katika maeneo ya Nanenane manispaa ya Morogoro wanasema wanaendelea vizuri na maandalizi kwa ajilia ya maonesho ya kilimo ya Nanenane yatakayofanyika kitaifa mkoani hapo.

Wamesema hayo walipokuwa wakizungumza na Gazeti la Msj weekly na kuongeza kuwa hii ni fursa ya pekee kwao na inabidi waichangamkie ili kuakikisha zoezi hilo linaenda vizuri ifikapo Tareha8/8/ mwaka huu.

Aidha Msj weekly iliweza kufunga safari mpaka kwenye viwanja yatakapofanyika maonesho ya kilimo Nanenane,na kuzungumza na Bw.Mwenyekida Tajiri ambaye ni mratibu na msimamizi wa bustani ya FARMBASE LIMITED iliyopo ndani ya viwanja hivyo vyamaonesho ya Mwalimu Julius Nyerere Nanenane

Mwenyekiti huyo alisema Fambase shiriks linalojishugulisha na kuuza, kusambaza madawa ya mimea ,mifugo pamoja na uuzaji wa vyakula nya mifugo.Ameongeza kuwa kwa sasa wapo wanaendelea kujiandaa vizuri kwasababu mwaka huu watatumia Teknolojia za kisasa zikiwemo za Green house na Drip irrigation.

Bw.Mwenyekida aliendelea kusema kuwa wanaipongeza serikali ambayo inaendelea kuwapa sapoti na mchango mkubwa wa viwanja na kuwafanya waendelee kufanya kazi zao vizuri. Akitaja faida amesema kuwa kutokana na kupata wateja wengi wakati




*Moja ya vitalu vya kuandalia miche ya mbogamboga za majani,kwa jina maarufu 'Green house' picha na Linus*

wa maonesho inapelekea kuuza madawa ya mimea na vyakula vya wanyama kwa wingi hivyo kupata fedha za kuendeshea mradi wao.

Hata hivyo aliweza kubainisha baadhi ya changamoto wanazozipata amesema kuwa wakulima wanapochelewa kuchukua miche ya mboga atimaye zinakomaa zikiwa kwenye bustani na kupelekea kupata hasara.

Hivyo kwa mwaka huu tumejiandaa sawasawa ili kuakikisha wakulima na wote wanaohitaji miche wafike mapema ili kuchukua miche mapema kabla haijakomaa.Swala ilo litasahidia kupunguza hasara wanazozipata endapo miche hiyo itakomaa ikiwa kwenye vitalu .

Ikumbukwe kuwa maonesho kwa mwaka yatafanyika ndani ya viwanja vya maonyesho ya mwalimu Julias Nyerere na maandalizi yakiwa yanaendelea kupamba moto sehemu zote ndani ya viwanya hivyo vya Nanenane Morogoro .

*TANGAZO TANGAZO*

- *Chuo cha uandishiwa habari Morogoro {MSJ]inatangaza nafasi za masomo kwa muhula wa kwanza,utakao anza mwezi wa saba na mwezi wa tisa Chuo kinatoa kozi zifiatazo;*
- *Basic foundation kozi kwa miezi 3*
- *Cheti chajuu cha uandishi wa habari [astashahada ]kwa mwaka mmoja*
- *Stashada ya uandishi wa habari kwa miaka miwili*
- *Chuokina patikana ndani ya viwanja vya maonyesho vya mwalimu Julius Kambarage Nyerere nanenane*
- *Ada zetu ni nafuu na utalipa kwa awamu ,*
- *Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi kwa namba*
- *0673131192*
- *Barua pepe Msj72 @ymail .com.*

*WAHI SASA NAFASI CHACHE*

## Ajira kwa watoto kikwazo Mkoani Morogoro

Morogoro

Wazazi na walezi washauriwa kuwapeleka watoto wao shule pale wanapofikisha umri unaoruhusu na kuacha tabia iliyozooeleka ya kuwatumia katika shughuli za uzarishji.

Hayo yamebainishwa na wadau wa elimu baada ya wazazi waliowengi katika kata ya Tungi,Mtaa wa Nanenane manispaa ya Morogoro mkoani humu kuwatumia watoto wao katika shuguli za uzalishaji hasa biashara na waengine kuchoteshwa maji huku wakiwa na umri unawaruhusu kuwa shule.

Aidha watoto hao wenye umri kati ya miaka 7 mpaka 11 ambao majina yao yameifadhiwa kutokana na kuwa na umri mdogio wamesema katika nyakati tofauti kuwa wazazi wao wamekuwa wakiwalazimisha kufanya biashra hizo na kuwakataza wasiende shule swala linalowafanya wakose masomo yao kwa muda mrefu na kusababisha wafanye vibaya katika mitihani yao.

Katika hali nyingine watoto hao wameonekana kuwa katika hali mbaya ya kiafya na kuvaa mavazi yaliochakaa na machafu japokuwa wazazi wao wanawatumia katika shughuli za uzalishaji na ujasiliamali,hali hii ikiwa ni kinyume na haki za watoto.

Pamoja na hayo wadau wa elimu wameonesha kukerwa, hivyo kukemea vitendo hivyo na kuongeza kuwa mtoto anapaswa kupata mahitaji yake yote ya msingi hasa elimu na si wazazi kuwabakiza nyumbani na kufanyisha kazi zinazotakiwa kufanywa na wazazi wenyewe.



*Mtoto akiwa anafanya biashara*
*picha na Hemedi*

Wadau hao na viongozi mbalimbali katika maeneo haya wameelekeza kilio na masikitiko yao kwa serikali na kuiomba kuwashughulikia wazazi na walezi wanaowafanyia vitendo hivyo kwa watoto vilevile kuweka sheria kali na kufanya ufatilizi wa kina mpaka katika mazingira wanakotokea watoto hao kwa kufanya hivo wanweza kukomesha vitendo hivyo wanavyofanyiwa watoto.

Nilazima tujitoe kufanya kazi yakuwaelimisha jamii kuhusu watoto wa mitaani Mkoani Morogoro

## Ubovu wa barabara changamoto kwa Bodaboda

Waendesha pikipiki halimaalifu kama Bodaboda wa maeneo ya mtaa wa Nanenane kata ya Tungi-mkoani Morogoro wamesema kuwa wanafanya kazi hiyo ya kusafirisha abiria katika mazingira magumu kutokana na kuharibika kwa miundombinu ya barabara.

Akiongea na gazeti la Msj weekly kwa niaba ya waendesha bodaboda wenzake Bw.Frenk Jonasi amesema kuwa"waendesha Bodaboda wamaeneo ya Nanenane wamekuwa wakifanya kazi hiyo ya ujasiriamali katika hali ngumu kutokana na kuharibika vibaya kwa barabara hasa inayoanzia maeneo ya Nanenane ,Tubuyu mpaka Tungi".

Bw.Frank ameongeza kuwa barabara uharibika hasa kipindi hiki cha mvua za masika hali inayosababisha kufanya kazi katika wakati an mazingila mugumu hivyo kufanya kipati chao kupungua kwasababu Abilia wanaogopa kutumia usafiri huo kwa kuogopa kupata ajari.

Aidha wakatoa kilio chao kwa serikali kuwa watafurahi kama watatengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha rami au changarawe ili waweze kufanya kazi hiyo kwa urahisi kwasababu ni kazi kama kazi zingine na kuongeza kuwa ,kuna baadhi ya vijana wanashinda wakizurura ovyo pasipo kufanya kazi nao wanasababisha kukwamisha maendeleo na kuiomba serikali kuwachukulia hatua kali. Pamoja na hayo wameongeza kuwa kuharibika kwa miundombonu hiyo imesababisha kutokea kwa ajali katika barabara hiyo.

# Zijue faida za Mbogamboga

**Na.Mathew Mtaba**

Kilimo ni hazina katika nchi yoyoe mali hiyo ina manufaa kwa mtu binafsi na kwa taifa kwa ujumla.Nchi yetu ya Tanzania ina kilimo cha aina nyingi ,baadhi ya vilimo hivyo ni vya mboga mboga na matunda na chakula.

Hii leo tunakuletea kilimo cha mboga mboga hasa tunaangazia zaidi kilimo cha mchicha,kabichi na Chinese ambavyo ndivyo vinatajwa nqa wtu wengi kuwa ndiyo mboga maarufu na inzaalishwa kwa wingi katika nchi ya Tanzania. Tunaanza na zao la mchicha,Mchicha ni zao ambalo hulimwa kwa wingi sehemu yenye udongo wa ufinyanzi na utifutifu kwa mkoa wetu wa Morogoro hasa Morogoro mjini zao la mchicha hulimwa sana maeneo ya mji mpya,kichangani na maeneo mengine ambayo yamepitiwa na mito au sehemu nyingine zenye maji mengi. Mchicha umegawanyika katika sehemu kuu mbili nazo ni mchicha wa asili na mchicha wa kupandwa,Mchicha wa asili ni ule ambao umeota bila kupandwa na mwanadamu ambao jina lake maarufu huitwa mchicha bwasi na mchicha uliopandwa na mwanadamu umegawanyika katika makundi tofauti upo unaoota baada ya siku saba na siku tano. Mchicha ambao majani au maua yake hutumika kama chakula hutibu magonjwa yafuatayo kuuma mgongo,unatibu figo,tezi shingo,kusafisha njia ya mkojo,kusafisha damu,dawa ya kikohozi na inasaidia kupata haja kubwa kwa wingi . Msomaji wa makala hii nakushauri sana utumie mboga hii ya mchicha kwa ajili ya kuimarisha afya yako ili uweze kuwa mtu makini katika taifa hili,pia tutunze vizuri ardhi yetu na vyanzo vya maji kwa ajili ya kuweza kustawisha mboga zilizo bora kwa manufaa ya watu walio sasa na baadae hiko ndicho kilimo cha mchicha hiyo ndiyo mboga bora kwa mwanadamu.




*Kilimo cha Mbogamboga kwakutumia njia za kisasa*

Kabichi ni zao ambalo ustawi zaidi katika mikoa ya Arusha,Kilimanjaro,Morogoro,Tanga,Iringa na Mbeya.kabichi ina madini aina ya chokaa,protini na maji kwa wingi ,mboga hii inaweza kuliwa bila kupikwa au kuchemshwa kwa kutengenezwa kachumbari pia inaweza kupikwa pamoja na vyakula kama vile mahargwe na nyama. Kabichi ni zao ambalo upendelea zaidi hali ya baridi zao hili hustawi na kutoa mazao mengi na bora zaidi kwenye sehemu zenye miinuko ya kuanzia mita 1200 hadi 1900 kutoka usawa wa bahari zao hili ustawi zaidi katika udongo wa kitifutifu na wenye rutuba nyingi na uwezo wa kuhifadhi unyevu kwa muda mwingi vilevile linaweza kustawi katika aina mbalimbali za udongo ilimradi udongo huo usitwamishe maji na usiwe na chumvi nyingi. Endapo udongo hauna rutuba ya kutosha uongezewe mbolea za asili kama mbolea ya samadi na vunde,kabichi zinazolimwa hapa Tanzania ni prize druntied ambayo vichwa vyake ni vikubwa kilo 2 mpaka kilo 2 na nusu na ni bapa ambayo huchelewa kukomaa siku 110 hadi 120 tangu kupandikiza miche na hupasuka kirahisi aina hii huvumilia hali jua kali Copenhagen market,vichwa vyake ni vya mviringo na hupasuka kirahisi aina hii pia hukomaa mapema siku 90 hadi 100 tangu kupandikiza miche Groly of enkhiuzen,vichwa vyake ni vya mviringo hii huvumilia hali ya jua kali lakini huchelewa kukomaa siku 100 hadi 120 tangu kupandikiza miche na havumilii hali ya kupasuka.Aina nyingine ni Brunswick na Danish ball head. Kabichi ni zao linalotumia virutubisho vingi aridhini kulinganisha na mboga zingine.Hivyo kabla ya kustawisha panda mazao jamii ya mikunde ili kuongeza rutuba,Halikadhalika baada ya kuvuna panda mazao yanayotumia chakula kidogo kama vile karoti hubadilisha mazao pia hupunguza kuenea kwa wadudud waharibifu na magonjwa. Mbegu za kabichi huanza kuoteshwa kitaluni na baadae miche huamishiwa shambani ,lima vizuri sehemu itakayooteshwa mbegu,weka mboleaza asili zlizooza vizuri kiasi cha ndoo 5 hadi

**Inatoka uk>>..8**

10 zenye ujazo wa lita 20 kwa eneo la mita mraba 10.Changanya vizuri mbolea na udongo kasha lainisha udongo kwa kutumia reki.Baada kulainisha udongo tengeneza tuta lenye nafasi ya sentimita 10 mpaka 15 kutoka mstari hadi mstari. Funika mbegu kwa udongo au mbolea laini kasha tandaza nyasi kavu ili kuhifadhi unyevu,mwagilia maji kila siku asubuhi na jioni mpaka mbegu zitakapoota ,miche huwa tayari kwa kupandikizwa shambani baada ya majuma 3 hadi 5 tangu kuoteshwa. Kabichi hukomaa na kuvunwa baada ya siku 60 hadi 120 kutegemea aina iliyostawishwa tangu kupandikizwa miche. Chinese ni moja kati ya mazao ya mboga mboga inayolimwa sana nchi Tanzania,asili yake ni China na baadae ikasambaa dunia nzima.Chinese inakuwa vizuri kwenye jotolidi 18 hadi 22,zao hili linategemea maji mengi wakati wa ukuaji na linakua vizuri kwenye udongo wa kichanga na wenye unyevunyevu wa kutosha,wakati unaandaa shamba udongo utifuliwe vizuri kabla ya kupanda na andaa shamba wiki 6 kabla ya kupanda . Jinsi ya kuandaa kitalu kinatakiwa kiwe na upana wa mita 1 na urefu wa mita 5.Kitalu kinatakiwa kiwe na kingo ili kuzuia maji kutoka nje ya kitalu kasha panda mbegu kwenye kitalu kwa sentimita 15 hadi 20 mstari hadi mstari. Tumia mbolea ya kuku,mbuzi na nguruwe,tumia ndoo katika kila kitalu chenye mita 5 na pia weka mbolea ya

Kukuzia ya UREA kwa kila kitalu pale mmea unapofikia majani 5.Chinese hukoo baada ya miezi 3 hadi 4 inategemea na aina.Vuna kwa kutumia kisu au mkono,maisha ya Chinese ni mafupi sana tofauti na mboga zingine,hivyo unatakiwa kusafisha na pia baada hapo unaweza kutunza kwenye friji ili kuzuia kukauka.na hizo ndizo mboga mboga zinazosababisha mwanadamu kukua vizuri bila kupatwa na magonjwa.

## Jinsi ya kupika pilau la mayai

Pilau la mayai ni chakula kinacholiwa sana Tanzania bara na visiwani kwani ni chakula chenye radha ya kipekee nani chakula kitamu.

Mahitaji mchele,mayai,vitunguu swaumu na maji iriki viungo vya pilau na mdalasini maji safi na salama

Vifaa vinavyohitajika katika chakula chetu sufuria sufuria,mwiko,mfuniko,jiko, mafutayakula,

Unawasha jiko lako kisha unabandika maji tayari ya kwa kuchemsha mayai inategemea na kiasi gani unapika kwa Leo tutatumia kipimo cha mchele robo hivyo tutachemsha mayai matatu

Ikiwa mayai yanachemka unachambua mchele kisha unauosha na kuuweka kwenye chombo kisafi kisha kisha unamenya vitunguu swaumu na kuvitwanga kisha unaviweka pembeni na kukatakata vitunguu maji navyo unaweka pembeni kisha unatwanga iriki pamoja na mdarasini kisha unaweka pembeni baada ya hapo dk tano zitakua zimetimia

Unaipua mayai yako na kubandika maji ya moto yakisha chemka unabandika sufuria safi kisha unamimina mafuta kiasi baada ya dk kadhaa mafuta kupata moto unaweka vitunguu maji vitunguu vikisha chemka na kubadilika ranging kua ya gilgilani unaweka vitunguu swaumu baada ya hapo unaweka mdalasini Na viongo vya pilau baada a dk tano kuchemka unaweka mayai unachanganya mpaka mayai yawe ya gilgilan ndipo unayatoa na kuweka pembeni

Kisha unaweka mchele na kuukaanga baada ya dk tano unaweka maji ya moto ambayo hapo mwanzo ulikwisha yachemsha baada ya hapo unafunika mchanganyiko wako na kuacha uive baada ya dakika kumi mchele wako utakua umeiva vizuri na utakuchukua mfuniko wako tayari kwa kupalia makaa juu ili wali wako upate kukauka vizuri.itunze ndoa yako sasa kwa kupika itunze ndoa yako sasa kwa kumfurahisha mumeo kwa chakula kitam

Basi baada ya dk tano utafunua mfuniko wako na kugeuza kisha utaufunika tena kwa kuweka yale mayai uliokwisha yakaanga kwa viungo hapo nyuma baada ya hapo utaacha tena dk tano msomaji wa safuu hii ya mapishi hapo utakua umemaliza kupika pishi lako hili la pilau la mayai hivyo utaweza kuandaa kwa kinywaji chochote kile

Basi hapo utakua umemaliza kupika wali wako wa mayai na kuwa tayari kwa kuliwa iwe asubuhi mchana hata



MOROGORO SCHOOL OF JOURNALISM
MEDIA FOR DEMOCRACY
Published by Morogoro School of journalism (MSJ), under student organization (MOSJOSO)

# Maji ni uhai

Na Linus Patrick,

``Mcheza kwao utuzwa ‘’si kwamba leo kuna mchezo wa wa mpira wa miguu ili mje kwa wingi kunishangilia bali leo nimekuja kuwapasha mambo mazuri yanayopatikana katika mkoa wangu uliobalikiwa na wenye kila aina ya kivutio. Mkoa wa Morogoro ni kati ya mikoa 30 ya Tanzania.Umepakana na mikoa ya Tanga ,Pwani, Lindi, Ruvuma,Dodoma na Arusha. Morogoro ina ukubwa wa kilometa za mraba 72,939 ambapo kuna wakazi 2,218,492.kwa mjibu wa sense ya mwaka 2012. Morogoro ni kati ya mikoa mikubwa Tanzania ukiwa na jumra ya wilaya sita jambo linalodhihilisha kuwa kuna mahitaji mengi ya uduma za kijamii hasa hasa maji. Ni ukweli usiopingika kuwa maji ni moja ya mahitaji muhimu kwa binadamu na viumbe vyote hapa duniani kwakuwa kitahalamu zaidi ya theruthi mbili ya mwili wa binadamu ni maji ambapo ni kati ya asilimia 55 mpaka 75. Halmashauli ya manispaa ya Morogoro inakabiliwa na upungufu mkuibwa wa maji kutokana na vyazo vyake vya maji kukabiliwa na ukame uliotokana na mabadiliko ya hali ya hewa na uharibifu wa mazingira unaofanywa na wananchi wanaolima kandokando ya vyanzo hivyo. Uku halmashauli ya manispaa ya Morogoro ikiwa inategemea vyanzo viwili vya maji ambavyo  ni Bwawa la MINDU na maji ya mseleleko vilivyopo katika safu ya milima ya ULUGURU. Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira{MORUWASA} kwa sasa



ina uwezo wa kuzalisha Lita milioni 34 za maji kwa siku,wakata yanaitajika maji Lita milioni 40 jambo linaodhihilisha wazi kuwa bado kuna upungufu mkubwa kwa watu wa manispaa hiyo. Maji kutoka katika vyanzo hivyo ndiyo yanayotegemewa na wakazi wote wa manispaa ya Morogoro,kwa hiyo ukosefu wa maji ya kutosha umesababisha kukwama kwa baadhi ya shughuli jambo linaweza kusababisha kushuka kwa uchumi kwa manispaa hiyo. Kwa wakazi wanaoishi maeneo ya Kola,Bigwa na Nanenane  wanaweza kukposa kwa kipindi kirefu na maji yanapotoka yanakuwa ni machafu,yana mizizi na harufu kama yamechotwa kwenye madimbwi,kitendo ambacho kinaweza kusababisha magojwa ya mlipuko kama Maleria. Jambo la kushangaza mamlaka inayohusika yaani{MORUWASA} wanakimbilia kudai bili ya na kukatisha huduma maji kwa wasiolipa ,wakatai yanapokatika huwezi kuwaona wakishugulikia swali hilo.


*TANGAZO TANGAZO*

- *Chuo cha uandishiwa habari Morogoro {MSJ]inatangaza nafasi za masomo kwa muhula wa kwanza,utakao anza mwezi wa saba na mwezi wa tisa Chuo kinatoa kozi zifiatazo;*
- *Basic foundation kozi kwa miezi 3*
- *Cheti chajuu cha uandishi wa habari [astashahada ]kwa mwaka mmoja*
- *Stashada ya uandishi wa habari kwa miaka miwili*
- *Chuokina patikana ndani ya viwanja vya maonyesho vya mwalimu Julius Kambarage Nyerere nanenane*
- *Ada zetu ni nafuu na utalipa kwa awamu ,*
- *Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi kwa namba*
- *0673131192*
- *Barua pepe Msj72 @ymail .com.*

*WAHI SASA NAFASI CHACHE*







Published by Morogoro School of journalism (MSJ), under student organization (MOSJOSO)

# Trump atoa msimamo wake vikwazo dhidi ya Iran



*Rais wa marekani Mh.Dornald Trump akizungumza na waandishi wa habari*

Rais Dornald Trump wamarekani amelegeza vikwazo dhidi ya Iran kutokana na mpango wake wanyuklia tofauti na msimamo wakati wa kampeni.

Hatua hii nikufuatia vikwazo dhidi ya Iran vilivyotolewa mwaka 2015 chini ya Rais Barack Obama akiungwa mkono na mataifa mengine matano yenye nguvu.

Wakati wa kampeni Trump alitishia kufuta makubaliano hayo ambapo Iran ilikuba likupunguza kiasi chake.

Trump amesema vikwazo zaidi vinahitajika kupambana utengenezaji wasilaha za nyuklia duniani.

Ameongeza kuwa Marekani itaweka pia vikwazo kwa maafisa pamoja na wafanyabiashara kutoka china ambao wanahusishwa na mpango wa nyuklia wa Irani.

# Ndege za China zazuia ndege ya Marekani

*Na.Mtandao*



Ndege ya kivita ikijiandaa kuruka

Ndege mbili za kijeshi za China zimeizuia 'vibaya' ndege ya Marekani kulingana na jeshi la Marekani.

Ndege hiyo inayohusika na kufanya uchunguzi, ilikuwa katika safari yake ya kutaka kugundua mionzi katika anga ya kimataifa iliopo mashariki mwa bahari ya China.

Ndege hiyo ilikuwa imetumiwa kugundua ushahidi kuhusu majaribio ya kinyuklia ya Korea Kaskazini.

China imekuwa ikituhumu vitendo vya Marekani karibu na maji hayo yenye utajiri mkubwa yaliopo katika pwani yake ,hatua ambayo imesababisha wasiwasi kati ya mataifa hayo mawili.

"Swala hilo linaangaziwa na China kupitia njia mwafaka ya kidiplomasia mbali na zile za kijeshi", msemaji wa jeshi la angani la Marekani Luteni kanali Lori Hodge amesema.

"Uzuizi huo haukufanywa kwa njia ya "utaalamu" kutokana na hali ya rubani wa ndege hiyo ya China ikiwemo kasi ya ndege zote mbili", aliongezea akisema uchungzi wa kijeshi unaendelea.

# Watu 60 wauawa kusini mwa Libya

Na.Mtandao

Habari kutoka Libya, zinasema kwamba takribani watu 60 wameuawa, katika mapigano makali kati ya makundi mawili hasimu, Kusini mwa nchi hiyo.

Msemaji wa kundi la Libyan National Army, amesema kuwa uwanja wake wa ndege wa Brak al-Shati, ulivamiwa.

Kundi moja linalojiita Third Force, linasemekana ndilo lililotekeleza shambulio hilo.

Eneo hilo limekuwa likiangaziwa pakubwa kutokana na taharuki inayotanda kati ya wanaounga mkono serikali inayotambuliwa na Umoja wa mataifa iliyoko katika mji mkuu Tripoli, na wapinzani wao.

Mapema mwezi huu, kamanda mkuu wa Libyan National Army, Khalifa Haftar, alikutana na kiongozi mkuu wa serikali iliyopo Tripoli, Bwana Fayez al-Sarraj, ili kujaribu kuzima uhasama unaotokota Kusini mwa nchi hiyo. Image caption Ramani ya Libya

Libya iliingia vitani baada ya kuangushwa kwa utawala wa hayati Kanali Muammar Gaddaffi mnamo Oktoba 20 mwaka 2011.

MFJ newz


# Baraza lapinga pendekezo la saa moja ya ngono Sweden

Na.Mtandao

Madiwani katika baraza la mji mdogo wa Sweden wamepinga muswada wa pendekezo la kuwapa wafanyikazi wa manispaa wanaolipwa, 'mapumziko ya kufanya tendo la ngono'

Per-Erik Muskos, diwani wa Övertorneå alipendekeza kuwapatia wafanyikazi hao mapumziko ya saa moja kila wiki kwenda nyumbani na kupata wakati bora wa kujamiana na wapenzi wao. Aliambia BBC lengo kuu lilikuwa kuimarisha uhusiano baina ya watu. "Ni jina la herufi tatu{Sex} , "Bw Muskos aliposema mwezi Februari , akipuzulia mbali pendekezo la kwamba anaingilia maisha ya watu binafsi. Lakini wanachama wa baraza hilo ambao ni wahafidhina walipinga wazo hilo.

Meya wa Övertorneå, Tomas Vedestig, alihitimisha kwa kusema maisha ya kibinafsi ya wafanyikazi yanastahili kuwachwa vile yalivyo. "Si kazi ya baraza kuingilia," aliambia SVT. Bw Muskos alitumai kwamba kichwa cha mpango wa unyakuaji ungeongeza idadi ya watu katika mji wake ambao kwa hivi sasa idadi hiyo imezidi kushuka.



*Per-Erik Muskos, diwani wa Övertorneå alipendekeza kuwapatia wafanyikazi hao mapumziko ya saa moja kila wik*

Mji wa Övertorneå kwa hivi sasa ni eneo ambalo lina watu 4,500 lakini wengi wao ni mwenye umri wa wastani.

' 'Vijana wengi huondoka mji huo pindi tu wanapo kamilisha masomo yao ,"Kasela amesema. Pia anadhani kwamba kutenga saa moja kwa wiki kutawasaidia wanandoa ambao hawana wakati na wapenzi wao.

' 'Watu wana vitu vyengine vingi vya kufanya ," alisema. Ukiwa nyumbani watu wako kwenye mitandao, unahitajika kuwapeleka watoto kushiriki katika michezo ya soka na mpira wa magongo ya barafu , watu hawana wakati wa kulinda kila mmoja na kuwa na wakati bora bila watoto. Iwapo wafanyikazi wa 550 wa baraza wamekasirika, itakuwa afueni kupata njia ya kutoa hasira katika hali hiyo mbaya: kwa sasa wana saa moja kwa wiki kushiriki katika michezo tofauti.

MFJ newz

# Waziri wa zamani afaulu mtihani akiwa na miaka 82 India

Waziri wa zamani ambaye anatumikia kifungo gerezaji baada ya kupatikana na kosa la kula rushwa amefaulu mtihani wa kumaliza shule India akiwa na miaka 82. Om Prakash Chautala, aliyehudumu kama waziri mkuu wa jimbo la Haryana kaskazini mwa India kwa mihula minne, alifanya mtihani wa darasa la 12 akiwa katika jela ya Tihar mjini Delhi.

Mwanawe wa kiume Abhay Chautala alisema babake aliamua "kutumia vyema muda wake gerezani".

OP Chautala alipatikana na makosa kuhusiana na kuajiriwa kwa walimu.

Abhay Chautala aliambia gazeti la Indian Express kwamba babake amekuwa kila siku akienda kusoma katika maktaba ya gereza hilo. Husoma magazeti na vitabu. Huwa anawaomba wafanyakazi wa jela kumtafutia vitabu avipendavyo zaidi. Husoma vitabu kuhusu wanasiasa maarufu duniani,2 amesema.

Bw Chautala na 54 wengine, walipatikana na hatia ya kughushi vyeti walipokuwa wanwaajiri walimu 3,206 kati ya 1999 na 2000. Waendeshaji mashtaka walisema watu waliokuwa wamehitimu zaidi walikataliwa na badala yake wale waliokuwa wametoa hongo wakaajiriwa.




*Baadhi ya waandishi wa habari wakiwa katika maandamano siku ya uhuru wa nyombo vya habari Mkoani Morogoro.* *Picha na Mathew Mtaba*



*Kitalu cha mahindi ya kisasa kilichopo katika viwanja vya maonesho ya Nanenane Morogoro.*
Picha na Saleh K.Mzee



*Barabara ya Nanenane Morogoro iliyo-haribiwa na mvuia*
*Picha na Husina Said*


Published by Morogoro School of journalism (MSJ), under student organization (MOSJOSO)

## Wachezaji watano wateuliwa kuwania tuzo ya uchazaji bora VPL




Wachezaji watano wameteuliwa (nominees) kuwania tuzo ya Mchezaji Bora wa Ligi Kuu ya Vodacom kwa msimu wa 2016/2017.

Walioteuliwa kuingia kwenye kinyang'anyiro hicho ni Aishi Manula (Azam FC), Haruna Niyonzima (Yanga), Mohamed Hussein (Simba), Shiza Kichuya (Simba) na Simon Msuva (Yanga).

Majina hayo yatapigiwa kura na makocha, makocha wasaidizi na manahodha wa timu za Ligi Kuu ya Vodacom pamoja na wahariri wa michezo kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini.

Wahusika watatumiwa fomu maalum za kupiga kura kwenye email za klabu zao na vyombo husika vya habari. Mwisho wa kupiga kura ni saa 6 usiku ya Jumanne, Mei 23 mwaka huu.

Hafla ya kutoa tuzo hiyo ambayo inaratibiwa na Kamati ya Ushauri ya Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) itafanyika Mei 24 mwaka huu kwenye ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam.

## ZIDANE,RONALDO MCHEZAJI BORA



*Mchezaji wa Real Madrid Christian Ronaldo akiwa na tuzo ya mchezaji bora wa dunia* *picha na mtandao*

Kocha mkuu wa kikosi cha Real Madrid amesema mchezaji wa kikosi chake Christian Ronaldo anasitahili kuchukua tuzo ya mchezaji bora wa dunia wa mwaka msimu wa 2017-2018 kutokana na kiwango bora anacho kionesha sasaivi.

Mchezaji huyo amekuwa moto wa kuotea mbali katika michezo ya mtoano ya ligi ya mabingwa ulaya UEFA baada ya kufunga magoli nane katika michezo mitatu miwili ya robo fainali dhidi ya Bayern Munich na mmoja dhidi ya Atletico Madrid nakuisaidia timu yake kuingia fainali ya michuano hiyo.

Christian Ronaldo kama akichukua itakua ni tuzo yake ya tano katika maisha yake ya soka na ya pili mfululizo kwani msimu uliopita alichukua tuzo hiyo kwa kumpiku mpinzani wake wa karibu Lionel Messi wa Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye magoli 103 hadi sasa kwenye ligi ya mabingwa ulaya tu pia mchezaji huyo ameisaidia timu yake kufuzu fainali ya ligi ya mabingwa ulaya ambao watavaana na wababe wa Italia Juventus.

Timu ya Real Madrid imeingia fainali ya ligi ya mabingwa ulaya UEFA baada ya kuifunga Atletico Madrid kwa jumla ya magoli manne kwa mawili baada ya kushinda magoli matatu kwa sifuri katika mchezo wa kwanza na kupoteza mbili kwa moja ugenini katika mchezo wa marudiano lakini wakapita kutoka na faida ya ushindi walioupa katika mchezo wa kwanza nyumbani Santiago Bernabeu.

# MU-IVORY COAST KUCHEZESHA TANZANIA, ANGOLA



*Wachezaji wa timu yataifa chini ya miaka 17 Serengeti boys wakiwa mazoezini*
*picha na Hosiana*

Abou Coulibaly atachezesha mchezo wa pili wa Kombe la Mataifa ya Afrika kati ya Serengeti Boys ya Tanzania na Angola utakaofanyika Uwanja wa l'Amitie kuanzia saa 11.30 jioni kwa saa za Tanzania.

Mwamuzi Coulibaly atasaidiwa na Mamady Tere wa Guinea na Attia Amsaad wa Libya wakati mwamuzi wa akiba atakuwa Mohamed Maarouf wa Misri huku Kamishna akiwa ni Ismael Locate wa Reunion.

Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Bakari Nyundo Shime amesema kwamba ameiona Angola ikicheza na Niger katika mchezo wa kwanza uliofanyika mara baada ya mchezo wa Serengeti na Mali.

"Utakuwa ni mchezo wa ushindani. Nasi tunakwenda kushindana. Matokeo ya awali ya sare kwa timu zote mbili yanafanya mchezo huu kuwa mgumu kwa kundi B.

"Angola ni wa kuchungwa sana. Kwa sababu walipocheza na Niger waliweza kusawazisha mabao mawili kipindi cha pili. Hii inaonesha kuwa ni wepesi wa kusoma makosa yao na kujirekebisha.

"Ila kikosi changu kiko imara, nikiamini kwamba kesho nitapata matokeo mazuri. Watanzania waendelee kutuombea. Tutafanikiwa," amesema Shime maarufu kwa jina la Mchawi Mweusi.

# AS Monaco yatwaa ubingwa wa Ligue 1 baada ya miaka 17

WACHEZAJI wa AS Monaco wakishangilia baada ya usiku huu kutawazwa kuwa mabingwa wapya wa Ligue 1 kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2000,miaka 17 iliyopita hii ni kufuatia ushindi wao wa mabao 2-0 nyumbani Stade Louis II dhidi ya wageni wao Saint-Etienne.

Mchezaji bora chipukizi wa mwaka,Kylian Mbappe aliiandikia AS Monaco bao la kwanza katika dakika ya 19 kabla ya Valere Germain kufunga la pili katika dakika ya 93 na kuipa miamba hiyo ubingwa wake wa nane wa Ligue 1 na kuhitimisha ufalme wa mahasimu wao Paris Saint-Germain ambao wamekuwa wababe katika miaka ya hivi karibuni. REKODI



Msj


WEEKLY Sport

# Dani Alves,Bonucci waipa Juventus ubingwa wa tatu wa Coppa Italia




*Wachezaji wa timu Juventus wakishagilia ubingwa* *picha na Meshack Rutta*

MABAO ya dakika za 12 na 24 ya walinzi Dani Alves na Leonardo Bonucci yameipa Juventus ubingwa wa tatu mfululizo wa kombe la Coppa Italia baada ya Jumatano usiku kuifunga Lazio mabao 2-0 katika mchezo wa fainali uliochezwa huko Studio Olimpico,Roma.



ZIDANE: RONALDO MCHEZAJI BORA

Uk>>14

MOROGORO SCHOOL OF JOURNALISM

MEDIA FOR DEMOCRACY

Published by Morogoro School of journalism (MSJ), under student organization (MOSJOSO)